



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UCHUKUZI
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



TAARIFA YA HALI MBAYA YA HEWA KWA MWEZI SEPTEMBER NA OKTOBA, 2025

1.0 UTANGULIZI

Katika kipindi cha mwezi Septemba 2025 hali ya ukavu iliendelea kujitokeza katika maeneo mengi ya nchi ikiambatana na hali ya joto nyakati za mchana. Aidha, mwezi Oktoba, 2025 vipindi vya mvua vilijitokeza katika maeneo machache na kuashiria kuanza kwa msimu wa mvua za Vuli, hususan ukanda wa ziwa Victoria. Aidha, mtawanyiko wa mvua hizo haukuwa wa kuridhisha katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Hali hii ilisababisha ongezeko kidogo la unyevu ardini, kina cha maji na malisho kwa maeneo machache. Hata hivyo, vipindi vifupi vya upepo mkali vilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani, kati mwa nchi, nyanda za juu kusini magharibi na maeneo ya maziwa makuu. Hali ya hewa iliyojitokeza pamoja na athari zake imeendana na taarifa ya mwelekeo wa mvua za Vuli (Oktoba-Disemba), 2025.

1.1 Mvua kubwa kwa mwezi Septemba, 2025

Katika kipindi cha mwezi Septemba 2025, vipindi vya mvua vilijitokeza katika maeneo machache, hususan maeneo ya ziwa Victoria. Aidha, katika kipindi hiki hakuna vipindi vya mvua kubwa vilivyojitokeza nchini. Kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 44.2 ndani ya saa 24 kilipimwa katika kituo cha Bukoba (Mkoa wa Kagera) mnamo tarehe 15 Septemba, 2025.

1.2 Hali joto kwa mwezi Septemba, 2025

Katika kipindi cha mwezi Septemba, 2025 maeneo machache ya nyanda za juu kusini magharibi yaliendelea kupata vipindi vya baridi. Kiwango kidogo zaidi cha joto la chini cha nyuzi joto 5.4 °C kilirekodiwa katika kituo cha Uyole kilichopo mkoa wa Mbeya mnamo tarehe 6 Septemba, 2025.

Katika nyakati za mchana, viwango vya joto la juu viliongezeka kidogo katika baadhi ya maeneo nchini. Maeneo ya Mpanda (mkoa wa Katavi) yalikua na vipindi vingi vya joto ukilinganisha na maeneo mengine ambapo kwa siku 5, viwango vya juu vya joto vilikuwa nyuzi joto 35°C au zaidi. Kiwango cha juu zaidi cha joto cha nyuzi joto 36.6°C kiliripoti mnamo tarehe 30 Septemba, 2025 katika kituo cha Mpanda (Mkoa wa Katavi).

Jedwali 1. Idadi ya siku ambazo viwango vikubwa vya joto la juu vilijitokeza kwa mwezi Septemba, 2025

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe: met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)


Kanda	Kituo	Idadi ya siku (≥ 35°C)	Kiwango cha Joto la juu zaidi kurekodiwa (°C)
Magharibi	Mpanda	5	36.6°C
	Tabora	1	35.3 °C

1.3 Upepo Mkali kwa mwezi Septemba, 2025

Katika mwezi Septemba 2025, vipindi vya upepo mkali unaofika kilomita 40 hadi 50 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani (Mikoa ya Dar es salaam, Pwani, Tanga, Lindi, Mtwara pamoja na Visiwa vya Unguja na Pemba) pamoja na maziwa makuu (Ziwa Viktoria, ziwa Tanganyika pamoja na Ziwa Nyasa,)

1.4 Mvua kubwa kwa mwezi Oktoba, 2025

Katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2025 vipindi vya mvua vyenye mtawanyiko na mwendelezo usioridhisha vilijitokeza katika aeneo ya ukanda wa pwani na magharibi mwa nchi. Aidha, vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo vilijitokeza katika maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria ikiashiria kuanza kwa msimu wa mvua za Vuli, 2025. Ongezeko kidogo la mvua lilijitokeza katika maeneo ya mwambao wa pwani kuelekea mwishoni mwa mwezi, kutokana na mabaki ya mawingu mazito ya mvua ya kimbunga "CHENGE". Kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 193.2 kilipimwa katika kituo cha hali ya hewa Matangatuani, Pemba, mnamo tarehe 29 Oktoba, 2025. Vituo vilivyoripoti vipindi vya mvua kubwa vya milimita 50 au zaidi ni kama vinavyoonekana kwenye Kielelezo 1.



Kielelezo 1: Viwango vya mvua kubwa kwa mwezi Oktoba, 2025

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe: met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

1.5 Hali joto kwa mwezi Oktoba, 2025

Katika kipindi cha mwezi Oktoba 2025, hali ya joto ilienelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, hususan mikoa ya magharibi (Katavi na Tabora. Kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 35.2 °C kilirikodiwa katika kituo cha Mpanda (mkoa wa Katavi) mnamo tarehe 16 Oktoba, 2025. Mkoa wa katavi uliendelea kuwa na siku zenye joto zaidi ukilinganisha na mikoa mingine amabapo kwa siku 2 viwango vya juu vya joto vilifikia au kuzidi nyuzi joto 35 °C.

Jedwali 2. Idadi ya siku ambazo viwango vikubwa vya joto la juu vilijitokeza kwa mwezi Oktoba, 2025

Kanda	Kituo	Idadi ya Siku (≥ 35 °C)	Kiwango cha Joto la juu zaidi kurekodiwa (°C)
Magharibi	Mpanda	2	35.3 °C
	Tabora	1	35.2 °C

1.6 Upepo Mkali kwa mwezi Oktoba, 2025

Katika kipindi cha mwezi Oktoba, vipindi vya upepo wa wastani vilitawala maeneo mengi. Aidha, vipindi vichache vya upepo mkali unaofika kilomita 40 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani pamoja na maziwa makuu. Nguvu ya upepo mkali ilisababisha athari mbalimbali katika maeneo hayo.

Matukio haya ya hali mbaya ya hewa yanaonesha ongezeko la changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na umuhimu wa kutekeleza mikakati thabiti ya kukabiliana mabadiliko hayo ili kulinda jamii na mazingira.

Imetolewa: tarehe 17 Novemba, 2025

Na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)